TANGAZO LA SERIKALI Na. 50N Lililochapishwa tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA ITOKANAYO NA MIKOPO KUTOKA TAASISI ZA KIFEDHA ZA NJE KATIKA MRADI WA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA MTAMBO WA UKOBOAJI NA UFUNGASHAJI WA MCHELE WA KAMPUNI YA WILMAR RICE TANZANIA LIMITED YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Riba Itokanayo na Mikopo kutoka Taasisi za Kifedha za Nje katika Mradi wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Mtambo wa Ukoboaji na Ufungashaji wa Mchele wa Kampuni ya Wilmar Rice Tanzania Limited ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 3 Julai, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio kwenye riba itokanayo na mikopo kutoka taasisi za kifedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Mtambo wa Ukoboaji na Ufungashaji wa Mchele wa Kampuni ya Wilmar Rice Tanzania Limited katika uanzishwaji na uendeshaji wa kuzalisha na kufungasha mchele inasamehewa.

Ukomo

**3.** Amri hii itafika ukomo tarehe 31 Mei, 2026 kwa mujibu wa kipengele cha 3.3 cha mkataba baina ya Kampuni ya Wilmar Rice Tanzania Limited na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*